# 1. Misingi ya viuawadudu

## Mada ya 1c

# Aina za viuawadudu


# JARIDA LA UHAKIKA


## 1. Misingi ya viuawadudu

## <u>Mada ya 1c:</u> Aina za viuawadudu

Kuna aina nyingi za viuawadudu. Aina tofauti za viuawadudu hudhibiti aina tofauti za viumbehai viharibifu. Vifuatavyo ni viuawadudu vinavyotumiwa sana:

| **Aina ya kiuawadudu** | **Hudhibiti** |
|---|---|
| **Viuawadudu wadogo sana** | Wadudu wote. |
| **Viua kuvu** | Kuvu (husababisha magonjwa mengi sana ya mimea). |
| **Sumu ya magugu** | Mimea isiotakikana, kama nyasi na magugu yenye majani mapana katika mazao. |
| **Viua utitiri** | Utitiri: kiumbehai kidogo kinachosababisha madhara makuu kwa mazao. |
| **Viua nematode** | Nematode: viumbehai vidogo udongoni vinavyovamia mizizi ya mimea. |
| **Viua moluska** | Konokono na koa |
| **Viua wanyama wagugunaji** | Panya na panyabuku. |






**MUHIMU :**
**Kila kiuawadudu kina aina yake ya viumbehai vya kudhibiti.**
**Huwezi kutumia sumu ya magugu kudhibiti wadudu wadogo.**
**Huwezi kutumia viua wanyama wagugunaji kudhibiti kuvu.**
**Jua viuawadudu vyako – Soma kibandiko cha maelezo – kuwa na busara!**

# MAELEZO YA ZIADA

## 1. Misingi ya viuawadudu

## <u>**Mada ya 1c:**</u> Aina za viuawadudu

Viuawadudu vinaweza kuainishwa kwa kutumia njia tofauti:

1. Kulingana na aina ya viumbehai viharibifu vinavyodhibitiwa (tazama makaratasi ya vitendo).
2. Kulingana na kundi la kemikali.
3. Kulingana na kiwango cha kusumisha (tazama mada ya 11b kuhusu jinsi ya kusoma ukanda wa sumu).
4. Kulingana na njia ya utendaji kazi: vile viuawadudu hufanya kazi.

Kujua migao tofauti ya viuawadudu kutasaidia mkulima katika kuchagua kiuawadudu kilicho bora.

# MWONGOZO

## 1. Misingi ya viuawadudu

## <u>Mada ya 1c:</u> Aina za viuawadudu

### Vifaa vinavyohitajika:

- ☑ Ubao ulio na makaratasi
- ☑ Markers (1 nyeusi, 1 bluu, 1 kijani, 1 nyekundu)
- ☑ Kadi za rangi
- ☑ Ukanda wa kubandikia

### Muda unaohitajika: Dakiki 30

### Maandalizi:

- ☑ Makaratasi ya kufungua kurasa yalio na kichwa: *Aina za viuawadudu*
- ☑ Karatasi kubwa lililo na jedwali lifuatalo:

| Aina za viuawadudu | Kiumbehai kiharibifu |
|---|---|
| | Wadudu wote wadogo |
| | Kuvu |
| | Mimea isiotakikana |
| | Utitiri |
| | Nematode |
| | Konokono na koa |
| | Panya na panyabuku |

## Mwanzo

**U**sikivu: Uliza washiriki: Ukiumwa na kichwa, unaweza kunywa dawa ya kukohoa? Watasema: La. Waulize: Ni nini unahitaji? Watajibu kwamba unahitaji dawa ya uchungu ili kutuliza maumivu ya kichwa.

**K**ichwa: Waambie kichwa: *Aina za viuawadudu.*

**K**usadikika: Elezea uzoefu wako katika viuawadudu.

**M**alengo: Kueleza aina tofauti za viuawadudu na jinsi vinavyotenda kazi.

**M**anufaa: Kuelewa vile viuawadudu tofauti hufanya kazi kutakusaidia kuchagua kiuawadudu sahihi kwa kila kiumbehai kiharibifu.

**M**welekeo: Katika kipindi hiki, tutaangazia aina tofauti za viuawadudu na jinsi vinavyotenda kazi.

# Wasilisho

## **U**fafanuzi, **M**aonyesho, **M**azoezi, na **M**wongozo:

1. Rejelea swali lako kuhusu jinsi ya kutibu maumivu ya kichwa. Waambie kwamba ni vivyo hivyo kwa viuawadudu na viumbehai viharibifu. Unahitaji kiuawadudu sahihi kudhibiti viumbehai viharibifu fulani.
2. Eleza kwamba **viumbehai viharibifu tofauti vinahitaji viuawadudu tofauti** kuvidhibiti. Gawanya washiriki katika vikundi sita. Waonyeshe jedwali lililo kwenye karatasi kubwa. Waambie kwamba mkulima dukani mwao ana kiumbehai kiharibifu cha kudhibitiwa. Taja viumbehai vyote vilivyo kwenye jedwali. Uliza yeyote kufafanua kuvu. Fafanua kuvu kwa ukamilifu. Fanya vivyo hivyo na utitiri na nematode.
    a. **Kuvu**: viumbehai kama mimea kama vile hamira, uyoga, na uyoga wenye sumu.
    b. **Utitiri**: Viumbehai vidogo sana vinavyosababisha madhara makuu kwa mimea.
    c. **Nematode**: viumbehai vidogo udongoni vinavyovamia mizizi ya mimea.
3. Sasa uliza vikundi kutafuta **aina sahihi ya viuawadudu** kwa kiumbehai kiharibifu kilioelezwa na mkulima. Waandike majibu yao katika madaftari. Wafanye kazi kwa dakika chache.
4. **Jadili** majibu/matokeo. Uliza kikundi cha kwanza kutaja aina ya kiuawadudu inayodhibiti wadudu wadogo. Uliza vikundi vingine kama vinakubaliana. Vikundi vyote vikikubaliana, ongeza jina hilo kwenye jedwali (au waweza kutumia kadi za rangi zilizotayarishwa na uzibandike kwa jedwali). Uliza kikundi kinachofuata kutaja aina inayodhibiti kuvu. Endelea hadi viumbehai viharibifu vyote vijadiliwe. Matokeo ya mwisho ni kama ifuatavyo:

| **Aina ya kiuawadudu** | **Kiumbehai kiharibifu** |
|---|---|
| **Viuawadudu wadogo sana** | Wadudu wote. |
| **Viua kuvu** | Kuvu |
| **Sumu ya magugu** | Mimea isiotakikana |
| **Viua utitiri** | Utitiri |
| **Viua nematode** | Nematode |
| **Viua moluska** | Konokono na koa |
| **Viua wanyama wagugunaji** | Panya na panyabuku. |

# Malizia

**M**uhtasari: Peana muhtasari kwa kutumia jedwali.

**M**aswali: Uliza kama kuna yeyote aliye na swali au maoni.

**T**athmini: Waulize aina za viuawadudu vinavyodhibiti: wadudu wadogo, kuvu, wanyama wagugunaji, magugu, na utitiri.

**H**atua fuatilizi: Katika kipindi hiki, tulijifunza kuhusu aina tofauti za viuawadudu. Wakati ujao mkulima atakapokuja dukani mwao na kiumbehai kiharibifu, watajua cha kupendekeza.

Sambaza **makaratasi ya taarifa ya maelezo** kwa washiriki wote.